Je! Kanisa Litaondoka Kabla ya Ile Dhiki?

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu wa maombi.

2 Mungu mtakatifu sana na mwenye haki, tunataka kukushukuru kwa ajili fadhili zako, kwa maana ni njema kwetu kuliko uhai. Nasi tunaomba ya kwamba utakutana nasi usiku wa leo katika njia maalum sana, na utupe baraka Zako. Naomba tuone mkono mkuu ulionyoshwa wa Mwokozi wetu mwenye upendo, kuwahudumia wagonjwa na kwa wanaoteseka. Na kuwasaidia wale waliochoka katika barabara ya dhambi, usiku wa leo. Kuwaalika katika nyumba ya Baba mahali ambapo wanatarajiwa kuwa.

3 Tungekuomba uwakumbuke wale ambao wameondoka kwenye njia nyembamba na iliyosonga, ili wao pia wapate kurudi kwenye ushirika wa Baba tena.

4 Nasi tunaomba, usiku wa leo, Bwana, ya kwamba Wewe utafungua maskio ya watu, kuisikia Injili, na ya kwamba utaitahiri midomo ya mnenaji. Na jalia tu tutumiwe kwa ajili ya utukufu Wako. Na mwisho wa ibada hii, tutakapoenda kwenye makazi yetu mbalimbali, hebu na tuseme kama wale waliokuja kutoka Emau, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo aliposema nasi njiani?" Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu Kristo. Amina.

5 Ningetaka kusoma baadhi ya Maandiko usiku wa leo, mlango wa 17 wa Luka Mtakatifu, na kuanzia ki—kifungu cha 26.

> *Na kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika siku zake Mwana wa Adamu.*
>
> *Walikuwa wakila na kunywa, walikuwa wakioa na kuolewa, hata siku ile Nuhu aliyoingia katika safina, gharika ikashuka ikawaangamiza wote.*
>
> *Na kadhalika, kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, walikuwa wakila na kunywa, walikuwa wakinunua na kuuza, wakipanda na kujenga;*
>
> *Lakini siku ile Lutu aliyotoka Sodoma kulikunya moto na kibiriti kutoka mbinguni vikawaangamiza wote.*
>
> *Hivyo ndivyo itakavyokuwa siku ile atakayofunuliwa Mwana wa Adamu.*

6 Na kwa somo, ninataka kuchukua kutoka Mwanzo, mlango wa 19 na ki—kifungu cha 22.

> *Hima, ujiponye huko, maana siwezi kufanya neno lo lote, hata uingiapo humo.*

7 Asubuhi ya leo, nilikuwa nikizungumza juu ya hukumu zijazo, na usiku wa leo ninataka kuendelea. Tunaweza kuhisi pepo zenye joto za hukumu inayokaribia ya Mwenyezi Mungu. Tunapoanza kuhisi mambo haya, inatupasa kwa namna fulani kuangalia mahali tunapoishi, na majira tunayopitia.

8 Na wakati fulani uliopita, nilibahatika kuizuru India. Na kabla tu ya kufika India, walipatwa na tetemeko kuu la ardhi. Nami nilikuwa nikisoma kwenye gazeti huko India, jinsi ambavyo yapata siku mbili kabla tetemeko hilo la ardhi halijatukia, ilionekana walijua kwamba kulikuwako na kasoro fulani; ndege wote wadogo wanaoishi kwenye mianya ya majengo makubwa, na walioishi kwenye kuta kubwa za mawe. Sehemu kubwa ya India wana kuta za mawe. Na ndege wote wadogo waliokuwa na viota vyao vidogo kwenye mianya hiyo, waliondoka kwenye hizo kuta. Na ng'ombe wote ambao kwa kawaida husimama karibu na majengo hayo makubwa, wakati wa alasiri, kwenye kivuli, na karibu na kuta hizo kubwa za mawe, kwa yapata siku mbili kabla ya tetemeko hilo la ardhi, wanyama hawa wote na ndege wadogo walitoka wakaenda katikati ya viwanja wakasimama.

9 Unaona, kulikuwako na kitu fulani kuhusiana na jambo hilo, kwamba Mungu alikuwa akishughulikia ndege Wake wadogo na wanyama Wake. Unajua, Mungu yeye yule aliyewaongoza kuingia kwenye safina, katika siku za mwanzoni, wakati walipoangamizwa na maji, katika mahubiri ya Nuhu, Mungu yeye yule angali anaishi na anatawala leo, naye anavitawala viumbe Vyake.

10 Nami nilikuwa nikiwazia, "Kama Mungu alikuwa anawajali sana ndege wake wadogo, na ng'ombe Wake na kondoo Zake, kuwaondoa kwenye maangamizi kabla hayajashuka, ni zaidi sana vipi Yeye anawajali watoto Wake ambao wamezaliwa kwa Roho Wake, wakaoshwa na Damu Yake. Yeye anawajali." Na kama vile alivyowaonya hao ndege wadogo watoke kwenye makazi yao, hakika ninaamini ya kwamba Yeye anawaonya watu Wake, leo. Tunapoona ishara kuu za Kuja Kwake kulikokaribia, ninaamini ya kwamba Mungu anawaonya watu Wake wakutanike pamoja, na mwito mkuu wa kutoka katika siku hii ya mwisho.

11 Somo langu usiku wa leo ni: *Je! Kanisa Litaondoka Kabla ya Ile—Ile Dhiki*?

12 Sasa wakati umeenda sana kuliko unavyofikiria. Wakati umeenda sana, hata ninaamini zaidi sana huku Marekani. Tuko kwenye mwisho wa barabara. Na asubuhi ya leo, wakati

nilipokuwa nikihubiri juu ya Babeli na hali zake, nilifikiri ingekuwa vyema sana usiku wa leo, kuingiza Biblia kidogo, kuonyesha jinsi gani tulivyo karibu na Kuja kwa Bwana. Nasi tunaweza kuona, sisi kwa jicho letu la kawaida, ya kwamba jambo fulani liko karibu na kutukia.

13 Kuna vu—vurugu kubwa miongoni mwa watu, ni vigumu tu kujaribu kuwa na ufufuo. Makanisa yanatofatutiana sana, na wanazozana sana, kwa sababu ya kuta za kimadhehebu. Nao Wakristo wana wasiwasi sana, inavyoonekana, na wamechanganyikiwa. Lakini, unajua, ni ajabu, bali Bwana wetu alisema, "Wakati mambo haya yanapoanza kutokea, tuangalie juu," ya kwamba ukombozi wetu unakaribia.

14 Na tunapoona rehema Yake iliyo kuu, wakati inapoonyeshwa kwetu sisi, tukiona mikono Yake ya ishara kuu na maajabu; ambazo, macho yetu yatafunguliwa, katika dakika chache, kuyaangalia. Na ndipo inatupa faraja hii nzito sana, kujua ya kwamba Mungu wa Biblia angali anaishi leo. Naye anawapenda watoto Wake, Naye anawapa onyo. Na wale ambao wana fahamu ya kiroho, wanatoka.

15 Na tunaona, katika siku ambazo Yesu alikuwa akinena habari zake, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na katika siku za Lutu."

16 Sasa, katika kila njia panda ya wakati, Mungu daima ametoa wito wa rehema kabla ya wito wa hukumu.

17 Sasa kama ninyi ni wanahistoria, nami nimekuwa nikisoma historia juma hili, na majuma mawili ama matatu yaliyopita, wale Mababu Waliotangulia Nikea, wa historia ya kale ya kanisa kabla tu ya lile Baraza la Nikea, na wakati huo walikuwa wakiunda kanisa Katoliki katika ile miaka elfu moja na mia tano ya nyakati zile za giza. Nami ninaona ya kwamba katika yale maandishi ya Nikea, ama lile Baraza Lililotangulia Nikea, ya kwamba mambo yalikuwa kama tulivyo leo. Loo, jinsi inavyojirudia!

18 Na kuona hali ya kanisa, na hali ya watu, na ishara za wakati, zimeandikwa kila mahali.

19 Sasa, kabla Mungu hajafanya jambo lo lote, kwenye kila njia panda ya wakati, Yeye daima hutuma rehema, malaika, nabii, Ujumbe. Na kama ilivyo kila wakati, hata sasa, yote yamedharauliwa. Kanisa halitaki kuupokea.

20 Nuhu. Yeye alinena juu ya Nuhu hapa. Naye alihubiri miaka mia moja na ishirini. Na ingawa ujumbe wake ulikuwa ni rehema, watu walishindwa kutilia maanani mafundisho yake. Ilikuwa ni kitu ambacho kingewaokoa, na hata hivyo hawangesikiliza. Na kama hiyo si picha nzuri sana ya siku hizi!

21 Sasa, unaweza ukaniambia, "Ndugu Branham, unawezaje kusema 'nzuri,' na huku kutuchorea picha ya mambo jinsi unavyotuchorea?"

22 Ni nzuri kwa sababu Bwana Yesu anakuja hivi karibuni kwa ajili ya Kanisa Lake, na ndilo wazo lililo zuri sana ambalo kiumbe cho chote cha Mungu kingeweza kuwazia; ili kutoka katika machafuko haya na kuingia katika Utukufu Wake uliobarikiwa, ambako wazee watakuwa vijana, na wagonjwa wataponywa milele. Hakutakuwako na huzuni wala machozi tena. Kama hilo si jambo zuri sana ninaloweza kuwazia! Na ni baraka jinsi gani kwa hao wanaongojea wakati huo wa kukusanyika.

23 Sasa tunaona, kama vile Yesu alivyorejea kwenye siku za Nuhu. Hebu na turudi nyuma tu, kwa sababu Yeye alisema, "Chukueni mfano wa siku hiyo."

24 Sasa, wakati Kaini na Habili. Wakati Kaini alipomwua Habili, na halafu Sethi akapachukua mahali pake. Tunaona ya kwamba Shetani alikuwa akijitahidi kuangamiza huyo Mzao aliyepaswa aje, ambaye Mungu alikuwa ameahidi, ya kwamba, "Mzao wa mwanamke utakiponda kichwa cha uzao wa nyoka." Naye Shetani alikuwa akijitahidi kumwangamiza huyo Mzao wa kifalme, naye alidhani amemwangamiza wakati alipomwua Habili. Lakini Mungu akamwinua Sethi mahali pake. Ni picha nzuri sana ya kufa na kufufuka kwa Kristo, na Mzao wa kifalme anayekuja.

25 Basi ni ajabu sana kuona jinsi ambavyo, katika upande ule wa Kaini, walikuwa ni wa kidini sana. Nao walikuwa ni watu wanaohudhuria kanisa; na vivyo hivyo Kaini alikuwa ni mtu wa kuhudhuria kanisa. Alimwabudu Mungu. Alijenga madhabahu. Alikuwa ni mfuasi wa kanisa. Alitimiza ahadi zake. Alikuwa, kwa kila hali kama vile mtu angeweza kumwangalia, alikuwa mwamini halisi.

26 Lakini kuna tabaka tatu za watu, hizo ni, waamini, wasioamini, na wanaojifanya waamini. Na ulimwengu ungali umejaa hao usiku wa leo.

27 Na kaini alikuwa ni mtu tu anayejifanya mwamini. Na kutoka katika ukoo wake kulitokea kundi kubwa la watu wanaohudhuria kanisa, watu wa kidini sana.

28 Sasa, jambo hili si la kawaida kabisa, bali je! uliona ya kwamba kutoka katika upande wake ilikuja jamii ya watu waliostaarabika, watu wenye elimu? Biblia inasema jambo hilo wazi wazi. Yeye alisema, "Walikuwa wakijenga, na walikuwa wakifanya mambo makuu." Sayansi ilitokana na ukoo wa Kaini. Na hao wanasayansi mashuhuri, na madaktari, na watu mashuhuri, walitoka kwenye ukoo wa Kaini.

29 Wakati, upande huo mwingine ulikuwa ni watu ma— maskini, watu aina ya wakulima wadogo wadogo, bali wao

walikuwa ni watu waliomwamini Mungu wao kuwa ni halisi. Ee Mungu, nihesabu pamoja nao!

30 Na kabla tu ya wakati wa mwisho kuja, kulitokea mchafuko mkubwa. Na ule upande mkubwa wa kanisa, ndivyo ilivyoonekana, walikuwa wameshinda, kama tu ilivyo siku hizi, kwa sayansi.

31 Na jambo lingine kubwa, yeye alisema, "Kulikuwako na ujenzi." Hakujatokea wakati katika historia ambapo ujenzi umekuwa mkubwa mno kama ilivyo sasa. Ni moja ya ishara za wakati wa mwisho. Hatujapata kamwe kuwa na wakati ambao watu wanajenga kama huu tulio nao. Na sasa, hata katika mji wetu mdogo hapa, siwezi kupata nafasi ya kutosha kwenda kuwinda sungura tena. Kote ni miradi ya ujenzi; ni kujenga tu na kupanda. Na kama tungeyafungua macho yetu, ni moja ya vibao vya matangazo ya Mungu ya kwamba ule mwisho umekaribia.

32 Na tulikuwa tunahubiri asubuhi ya leo, juu ya masputniki na makombora, jinsi wao wanavyoweza kusimama huko Moscow, na kuelekeza makombora kwenye Barabara ya Nne hapa Louisville, bila hata kuondoka Moscow. Na litachimba shimo ardhini, futi mia moja na sabini na tano kwenda chini, kwenye eneo la maili mia moja na hamsini mzunguko. Hivyo ndivyo ambavyo shimo hilo lingekuwa kubwa. Matatu ya hayo yangeuangamiza ulimwengu mzima, yautikise utoke kwenye mzingo wake. Sayansi, unaona iko upande gani? Iko kwenye upande wa uovu.

33 Mungu anataka watoto Wake kumwamini Yeye kwa kila jambo walilo nalo. Bali sisi tunataka kuutumaini mkono wa mwanadamu. Heri matumaini yangu yajengwe katika Kristo, nikichukua msimamo wangu wenye uchaji juu ya neema na rehema Zake, kuliko kundi lo lote la watu wenye elimu ambao wangeunda madhehebu, waseme, "Njia ndiyo *hii*." Kristo alisema, "Mimi ndimi Njia, Kweli, na Nuru. Wala hakuna mtu awezaye kuja kwa Baba Yangu ila kwa njia Yangu."

34 Kwa hiyo, unaweza kuona, ni siku kuu ya elimu. Ni siku nzito ya ugomvi duniani. Na papo hapo miongoni mwa hayo, hapana budi walikuwa na ulimwengu mkuu zaidi wa kisayansi kuliko tulio nao leo. Walijenga mapiramidi. Hatuna kitu hata kimoja kinachoweza kujenga piramidi, kama ungalipata kuwa karibu nalo. Nimekuwa karibu nalo, huko Misri, na yale yaliyoko Mexico. Na ni marefu sana, urefu wa majengo kadhaa ya mji, kungekuwa na majabali ambayo yangekuwa na uzito wa mamia kadha ya tani, yamejengwa huko juu ya jengo hilo kubwa, kubwa mno. Nayo yamechongwa kikamilifu sana mpaka hata hakuna nafasi kwa wembe; yalichongwa kwa ustadi mkuu. Loo, ni siku ya namna gani ya sayansi! Na, pia, limekaa kamilifu sana katikati ya dunia, na haidhuru jua liwe wapi, kamwe

hakuna kivuli kinacholizunguka. Nina shaka kama tungeweza kujilinganisha nao, siku hizi, katika sayansi yetu ya kisasa.

35 Lakini Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku ile, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Mungu." Sasa, na Nuhu alihubiri miaka mia moja na ishirini, na, angalia, alichekwa.

36 Sasa, Yesu pia alisema, ya kwamba, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, kwamba, ndivyo hali ingekuwa." Katika siku za Lutu, walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa, wakipanga, wakijenga, wakiuza, wakinunua.

37 Loo, hapajakuwako na siku, ambapo, biashara nyingi sana, kama ilivyo leo, maeneo mengi sana ya kuuzia magari ya mitumba na kila kitu. Kiasi kwamba, hata, unaweza kununua friji mwaka huu, na ulilipie kwa dola kama mia nne ama mia tano, na mwaka ujao hakuna mtu anayelitaka. Limepitwa na wakati. Je! huoni ambapo ulimwengu wa biashara unakutumikisha bila kupumzika? Unaweza kununa gari mwaka huu, na mwaka ujao labda ni zuri tu kama lile ungaliweza kununua wakati huo, lakini litapungua bei kwa dola elfu moja kwa sababu walibadilisha kifuniko cha rejeta ama wamelifanyia kitu fulani kidogo cha kipuuzi. Ni maneno tu ya kuvutia mnunuzi, kutimiza Biblia.

"Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na katika siku za Lutu."

38 Ingawa, kila wakati, malaika waliinuka, manabii wakainuka, na ujumbe wao daima ulikuwa ni neema, rehema, na ukombozi. Ujumbe wa Mungu daima umekuwa ni ukombozi, kabla tu ya wakati wa mwisho. Chunguza katika Maandiko. Jinsi Nuhu alivyohubiri ukombozi, nao waliwacheka na kuwadhihaki, na wakakejeliwa.

39 Na kama ilivyokuwa katika siku hizo, ndivyo ilivyo leo. Na wakati unapotoka kwenda na Ujumbe, ya kwamba Kristo amefufuka katika wafu, kama alivyoahidi angejionyesha Mwenyewe. Nao wanafanya jambo hilo leo, kwa ujumbe huo, kama tu walivyofanya kwa Ujumbe katika siku zile.

40 Lutu alitoka akaenda Sodoma, na akajaribu alivyoweza kuifanya jamaa yake isikilize ujumbe wa Malaika, bali walimdhihaki na kusema ya kwamba alikuwa anawatania.

41 Loo, ni picha ilioje ya siku hii! Wakati unapowaletea Ujumbe wa ukombozi wa Mungu, wao wanasema, "Unadhihaki dini. Unajaribu kuiga kitu fulani." Kundi la aina ile ile! Ni saa ya jinsi gani tunayoishi! "Vema, wanafikiri ya kwamba wao ndio tu watakaookolewa. Wanafikiri wao tu ndio wanaohubiri Injili."

42 Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Si neno Langu. Ni Neno Lake.

43 Pia angalia, ninataka uone, upesi, kwamba ulikuwa ni ujumbe wa aina gani. Loo, hili linausisimua moyo wangu. Ninapowazia juu ya Sodoma na Gomora, ilikuwa imepotoshwa sana, kimaadili, hivi kwamba wapotovu walijaa kila mahali.

44 Lakini kabla tu ya yale maangamizi makuu ya mwisho, Mungu alimtuma nabii sehemu zile. Na ninawazia pia juu ya, Yeye alimtuma Malaika kule, nami ninataka mwangalie Ujumbe wa Malaika huyo. Ibrahimu, ambaye alikuwa amechagua njia yake pamoja na watu wachache wa Bwana waliodharauliwa, alikaa huko nyikani ambako ardhi haikuwa na rotuba.

45 Naye Lutu alishuka akaenda akawa meya wa mji huo, naye alikuwa ni mtu mashuhuri katikati ya dhambi. Afadhali nisingependwa sana na watu, na niwe sawa kwa Mungu. Lakini Lutu alikuwa anapendwa sana na watu, naye aliketi mitaani, kwenye lango la mji. Alikuwa ndiye mwamuzi wa kile kinachoweza kuingia na kile kisichoweza kuingia. Naye huyo hapo, akiyatoa maisha yake kwa uzinzi, na akijua ya kwamba katika mji wake mambo kama hayo yalikuwa yanaendelea.

46 Kama hiyo si picha ya siku hizi, katika taifa letu; vipindi visivyokaguliwa, upuuzi wa kila namna, uhasama, hila! Loo, wangeweza kuvunjilia mbali kitu hicho, kama wangetaka, bali hawataki. Wala hawawezi kufanya jambo hilo, kwa kuwa Mungu alisema ingekuwa hivi. Laiti tu wangaliweza tu kufungua macho yao na kuweza kuelewa!

47 Na, angalia, kabla tu ya ile saa kuu ya uamuzi kufika. Ibrahimu na Sara, walioketi chini ya mwaloni, siku moja wakati wakiwa huko nje, Sara aliona Wanaume fulani wakija. Naye akakimbilia hemani.

48 Ni tofauti jinsi gani, kwa wanawake wa siku hizi, na ingekuwa ni tofauti jinsi gani kule Sodoma. Inapofika wakati wa wanaume kuja nyumbani, wote wanavaa nguo zao fupi, na wanatoka nje na kuchukua mashine ya kufyekea nyasi. Ni tofauti jinsi gani!

49 Lakini Sara alienda hemani. Na wakati alipoenda, Wanaume hawa wakaja. Ndipo Ibrahimu akawaangalia. Walionekana kidogo kama ni Watu wasio wa kawaida. Na mmoja wao alionekana kana kwamba ndiye kiongozi wao, na wakati Yeye alipoketi chini ndipo akaanza kuanza kuzungumza na Ibrahimu.

50 Ibrahimu akasema, "Ketini hapa, nami nitaenda kuwaletea maji, na nitawatawadhe miguu Yako. Halafu nitakanda mikate michache. Nasi tutakuwa tumeandaa, ndipo mnaweza kula nyama kidogo. Halafu mnaweza kuendelea na safari."

51 Na wakati alipokimbia kwenda kule kwenye kundi la mifugo, basi akamchukua ndama mnono, akamchinja. Akamwambia Sara akande unga kidogo na kutengeneza mikate michache.

52 Ndipo akazungumza na Mtu huyo. Ninaamini ya kwamba, kwa njia moja au nyingine, Ibrahimu alijua kwamba Huyo alikuwa ni nani. Na huyo Mtu aliyekuwa ndiye mnenaji, alikuwa ameelekeza mgongo Wake hemani. Alikuwa ndiye Mjumbe wa siku hiyo. Ndipo akasema, "Ibrahimu, nitakuzuru kulingana na ile ahadi, miaka ishirini na mitano hapo kabla. Nilikupa ahadi, nami nitaitimiza."

53 Loo, Jina la Bwana na libarikiwe! Mungu alitoa ahadi, "Katika siku za mwisho, Yeye angemwaga Roho Wake juu ya watu wote," naye atadumu nayo. Yesu alifanya ahadi, na kusema, "Mambo nifanyayo ninyi nanyi mtayafanya," Naye atadumu na hilo, kwa kuwa Yeye ni mwenye haki.

54 Ndipo Ibrahimu akamwangalia. Akasema, "Mnamo wakati kama huu mwezi ujao, wakati uu huu mwakani," hiyo ilikuwa kwa Sara, "Nitakuzuru, naye Sara atamzaa mtoto ambaye niliahidi." Sasa, Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka mia moja, na Sara alikuwa na tisini.

55 Naye Sara, akiwa yuko nyuma ya yule Malaika, ndani ya hema, akaninii . . . akacheka.

56 Na yule Malaika, akiwa amempa kisogo, akasema, "Kwa nini Sara amecheka?" Huyo alikuwa ndiye Mjumbe, [Ndugu Branham anagonga mimbarani mara saba—Mh.] Loo, hivi mnajua ninalozungumzia? Hiyo ilikuwa ni telepathia ya namna gani, huku ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, na huyo mwanamke akiwa yuko kule ndani? Naye mwanamke huyo akatabasamu. Ndipo huyo Mtu akasema, "Kwa nini amecheka?" Yeye alijua jambo hilo. Na huo ulikuwa ndio Ujumbe wa mwisho kabla ya Sodoma na Gomora kuteketezwa. Ndugu, kama ukiusikia Huo, usiku wa leo, sasa ni Ujumbe wa mwisho kabla ya ulimwengu huu kuchomwa moto. Unaona tabia ya Malaika huyo? Huyo Malaika alikuwa ni nani? Alikuwa ni Mungu.

57 Kumbukeni, Ibrahimu alimwita, "Bwana." Na tafsiri hapo ni "Elohim, Yule Yehova aliye mkuu, mwenye nguvu." Ilikuwa ni Yesu Kristo aliyefanyika mwili.

58 Mtu fulani alisema, "Unataka kuniambia ati huyo ndiye? Aliupataje ule mwili?"

59 Mbona, Yeye aliwaita tu hao Malaika wawili. Naye akapulizia pumzi kidogo, namna *hiyo*, ndipo atomi na kalisi na potashiamu zikaungana, na Gabrieli akaingia katika mmoja, na Malaika mwingine huo mwingine. Kisha Mwenyewe akajifanyia mmoja Yeye Mwenyewe.

60 Jina Lake takatifu na libarikiwe! Nina furaha sana, usiku wa leo, kujua ya kwamba Mungu yeye yule Mwenyezi, Ambaye aliweza kujifanyia mwili wa kuishi ndani, tumaini langu liko ndani Yake, ya kwamba siku moja Yeye atauinua huu, kama alivyoahidi kufanya.

61 Naye yuko miongoni mwetu, akifanya jambo lile lile alilotenda kule. Loo, Jina Lake tukufu na lisifiwe; akitupa onyo, akizungumza nasi, akitwambia tujitayarishe. Bila shaka, Yeye alisema, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Lakini, ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Ni saa ya jinsi gani tunayoishi!

62 Angalia, yule Malaika aliyeshusha moto huo, Ndiye aliyefanya huo muujiza. Nasi sote tunajua ya kwamba ulimwengu utaangamizwa, wakati ujao, kwa moto. Na yule Malaika aliyetumwa Sodoma na Gomora. . . Angalia kile Yesu alichosema. Loo, linasisimua tu nafsi yangu kulifikia jambo hilo. "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa wakati wa Mwana wa Adamu." [Ndugu Branham amegonga mimbarani mara saba—Mh.] Huyo Malaika alifanya nini? Alikuwa na roho ya utambuzi. Naye alisema, "Kama ilivyokuwa wakati huo, hivyo ndivyo itakavyokuwa wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa kutoka Mbinguni." Unaona jambo hilo? Wazia tu, ya kwamba, katikati yetu sasa amesimama Malaika yule yule wa Mungu, ambaye si mwingine ila ni Bwana Yesu Kristo, katika umbo la Roho Mtakatifu. Yuko miongoni mwetu, "Katika siku hiyo." Naye alikuwa ni Mungu, na huo ulikuwa ndio Ujumbe Wake kabla tu ya yale maangamizi kutukia.

63 Sasa tutaona ya kwamba ulikuwa ni Ujumbe wa ukombozi. Yeye alishuka kule na kujaribu kuwakomboa watu, nao walikataa kumsikiliza.

64 Na, leo, ni jambo lile lile katika taifa letu, miongoni mwa watu wetu. Nimepata majaliwa ya kumwona Bwana wetu Yesu, mikutanoni, akifanya ishara na maajabu na mambo makuu. Na watu kwa kweli watasimama mimbarani na kujua, bila shaka yo yote, ya—ya kwamba yule Mungu mkuu, asiyepatikana na mauti, asiye na kikomo yupo na anafanya mwujiza wa namna ile ile; na watu watasimama hapo na kutafuna chingamu, na kuondoka jukwaani, hawahusiki. Hawajali.

65 Kwangu mimi inaonekana, kana kwamba, kama mtu angekuwa na namna yo yote ya mambo ya kiroho kwake, ama na Roho wa Mungu ndani yake, na wakati anapomwona Bwana Yesu akitenda yale hasa aliyosema atafanya, ingemsisimua moyo wake hivi kwamba, hata asingeweza kujizuia tena. Angewasha taifa moto kwa Ujumbe huo. "Kama ilivyokuwa katika siku hizo," Yeye alisema, "ndivyo itakavyokuwa."

66 Huo ujumbe ulitangazwa, nao wakaucheka tu na kuufanyia mzaha, kama mtu aliyekuwa akisimulia hadithi ya uongo. Lakini ulikuwa ni wa rehema, na ulikuwa ni wa neema, na ulikuwa ni wa ukombozi. Loo, jamani!

67 Ndipo Malaika huyo akamwambia Lutu, asubuhi hiyo, baada ya kutoa ujumbe; Akasema, "Hima, ujiponye huko, maana siwezi kufanya neno lo lote hata utakapokuja huku." Ninawatakeni mwone jambo hili sasa, maana inatubidi kukatiza hapa, kwa ajili ya mstari wa maombi. Uliona vile yule Malaika alivyosema? "Siwezi kufanya neno lo lote hata utakapokuja huku." Ilikuwa ni kitu gani? Ulikuwa ni ujumbe wa ukombozi. Na kabla cheche moja ya moto kuanguka kutoka Mbinguni, ilibidi Lutu atoke Sodoma.

68 Na kabla tone moja la mvua halijashuka kutoka Mbinguni, Nuhu aliingia safinani.

69 Na kabla bomu la atomiki kupiga taifa hili, Kanisa litaenda katika Unyakuo, kumlaki Bwana Yesu. Na kama masputiniki na makombora yametegwa, na nyundo zimeinuliwa juu, Malaika wote wamesimama katika utaratibu. Haleluya! Kumbi kuu za Mbinguni zimejaa. Vinubi vyote viko tayari. Zile bendi kuu tayari zimefanyiwa mazoezi. Kuna Kurudi Nyumbani hivi karibuni, kwa ajili ya Kanisa la Mungu aliye hai, ambalo limekuwa likisubiri Kuja Kwake. Kila kitu kiko katika utaratibu. Nina furaha sana. Ninachoka sana. Loo, nina shauku ya wakati huo mkuu!

70 Na kuwazia, ya kwamba, tumekuwa na sehemu yetu katika njia panda ya wakati! Kumbukeni, "Ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu, wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa kutoka Mbinguni."

Sasa, kumbukeni, kabla mvua haijanyesha kutoka Mbinguni, Nuhu alikuwa safinani.

71 Kabla moto haujaanguka, Lutu alikuwa ametoka Sodoma. Kwa kuwa, yule Malaika alisema, "Siwezi kufanya neno lo lote hata utakapoingia huku. Nimeshika wenzo mkononi mwangu, wa kuvuta na kuufanya moto ushukue kutoka Mbinguni."

72 Nami ninafikiri hivyo ndivyo ilivyo hasa. Malaika wa maangamizi anaushikilia mkono wa Urusi, ulioshika mabomu ya atomiki; mpaka Kanisa la Mungu litakapoungana pamoja, na Mwili mmoja mkuu wa Kristo. "Siwezi kufanya neno lo lote hadi utakapoingia huku." Loo, kama hilo si dhamana iliyobarikiwa!

73 Na iwapo tunaona kila kitu kimewekwa katika utaratibu, kule kwenda Nyumbani kwa Kanisa kumeandaliwa tayari. Huyu hapa Malaika wa Mungu akiwa na Ujumbe ule ule, akifanya ishara zile zile, maajabu yale yale, kila kitu kimewekwa tayari. Enyi Maskani ya Branham, karibu miaka ishirini na mitano iliyopita, nilizungumza kwenye mimbara ii hii na kuwaambia mambo haya yatatendeka, moja ya siku hizi. Haya hapa! Tuko katika wakati wa mwisho. Njia panda iko hapa. Wakati wa Kwenda Nyumbani kwa Kanisa umekaribia.

74 Wakosoaji, wakitania, wakidhihaki, wakidharau, kama walivyofanya Mfalme Nebukadreza na Belteshaza. Ndivyo

binadamu alivyofanya katika siku za Nuhu. Ndivyo ilivyokuwa katika siku za Lutu. Nao wanafanya jambo lile lile leo.

"Siwezi kufanya neno lo lote hata utakapokuja humu."

75 Ninawatakeni mwangalie, Lutu alitoka katika kitu ambacho kingemwangamiza, na Nuhu aliingia kwenye kitu ambacho kingemwokoa. Na huo ni mfano wa Kanisa. Tumetoka ulimwenguni, na kuachana kwa mbali na wakati huu tunaoishi wa Elvis Presley na Arthur Godfrey. Tokeni ulimwenguni mwingie katika Kristo! Tumetoka ulimwenguni. "Hao ni wa ulimwengu, wataangamia pamoja na ulimwengu." Wale walio katika Kristo wataenda Nyumbani pamoja na Kristo. "Kwa maana wale waliolala katika Kristo Mungu atakuja pamoja nao wakati atakapokuja." Tumetoka ulimwenguni, kuingia katika Kristo kwa ajili ya usalama. Loo!

76 "Lakini siwezi kufanya neno lo lote hata utakapokuja humu." Ninapenda jambo hilo. "Hima! Ujisalimishe!" Ujumbe huo ulikuwa wa haraka. "Hima! Hima! Ujisalimishe!"

77 Jina la Bwana na libarikiwe! Yesu aliahidi Injili hii ingehubiriwa. Imekuwa ikiendelea sasa kwa miaka na miaka. Na ndiyo hii hapa kwenye wakati wa mwisho, ile ishara kuu ya mwisho. Kabla tu hao Malaika hawajasema kwa sauti kuu, "Hima," Yeye aligeuka na kusema, "Kwa nini Sara amecheka?" Malaika wa maangamizi, alisema, "Nimesikia kuhusu dhambi zao, nami nimekuja kuona kama ilikuwa ni kweli ama si kweli." Naye akakuta kwamba ilikuwa ni kweli. Na ujumbe huo ulikuwa wa neema, na rehema, na ukombozi. Lakini, "Hima! Hima!"

78 Loo, enyi watoto, msiketi mmeinama na kushangaa. Hima! Hima! Upesi! Wakati umekaribia. Kimbilieni (wapi?) huko nje kama wale ndege wadogo walivyofanya, nendeni mbali na hizi kuta za kisasa za Babeli, haya madhehebu makubwa ya kale yanayosema, "Hakuna tofauti ya wakati." Makanisa haya makubwa ya kale yasiyoamini yanayosema, "Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Hakuna miujiza." Ondokeni kwenye kuta hizo, kwa maana zitaanguka. Zitaanguka katika maangamizi na kushindwa, maana Mungu wangu alisema hivyo.

79 Kimbieni mkaingie katikakati ya kule Kalvari! Kama wale ndege walienda kwenye miti, nanyi pia endeni kwenye mti, ule mti ambapo Kristo alisulubiwa. Mkaning'inie huko katikati ya rehema Zake, mkamlilie Mungu hata dhoruba itakapopita.

80 Hima! Jisalimishe! "Njoo huku, kwa maana siwezi kufanya neno lo lote hata utakapotoka." Yeye anakungojea. Ondokeni kwenye maskini vitu hivi vya kisasa. Ondoka kwenye hiyo televisheni wakati michezo ya aina hiyo inapoanza. Ondo-. . . Funga redio wakati roki inapoanza. Enenda kama bibi. Vaa kama bibi. Enenda kama mwanamume. Vaa kama mwanamume. Zungumza kama Mkristo. Ishi kama Mkristo.

Unguza madaraja yote. Hima! Tokeni! Maangamizi yanakaribia. Mungu amechefuka moyo na amechoka.

81 Loo, muda umeenda sana kuliko mnavyodhania. Saa imewadia. Rehema ya Malaika, yule Malaika wa rehema Ambaye alituma Ujumbe Wake, yuko papa hapa usiku wa leo. Mnaaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Je! itabidi Kanisa kuondoka kabla ya wakati wa Dhiki? ["Amina."]

82 Angalia. Israeli walienda Gosheni; nayo Misri ikaingia katika giza. Misri iliingia Gosheni, wakapelekwa kwenye nchi ya ahadi. Misri ikaingia katika giza, na wakazikwa katika Bahari ya Shamu.

83 Hima! Hima! Ujisalimishe! Huenda hiyo ikawa ndiyo nafasi yako ya mwisho. Pia kumbuka, tunaona makombora yamewekwa. Tunawasikia, tunayaangalia gazetini. Ulimwengu mzima unatetemeka. Kila kitu ambacho Mungu alisema kitatimia.

84 Basi vipi kuhusu jambo hilo? "Katika siku ambayo Mwana wa Adamu atajifunua kutoka Mbinguni." Mwana wa Adamu ni nani, ambaye amefunuliwa? Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Angalia kwenye kifungu cha 21, ama kifungu cha 30, ndicho hicho.

> *Ndivyo itakavyokuwa katika siku zile atakapofunuliwa Mwana wa Adamu* kutoka mbinguni.

85 Ni kitu gani? Jumbe hizi ambazo. . .Jambo hili halijatukia kamwe tangu Yesu alipokuwa duniani. Na hili hapa, katika mwisho wa wakati wa Mataifa. Hebu na tuliangalie jambo hilo kwa muda kidogo tu, na tufikirie sana.

86 Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, Yeye hakudai kuwa mponyaji. Alisema, "Si Mimi ninayefanya kazi hizo; ni Baba Yangu. Bali ninafanya tu yale Baba anayonionyesha kufanya." Yohana Mtakatifu 5:19, Yeye alisema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda."

87 Kama ukimwangalia Filipo, wakati alipoongoka mara ya kwanza. La. . .Alipoanza huduma Yake, Bwana Yesu, ni nini kilitukia?

88 Hebu na tuone jinsi Mwana wa Adamu atakavyojifunua Mwenyewe. Kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, itambidi kujifunua Mwenyewe kama alivyofanya jana. Kama akijifunua vile vile, itambidi kufunua Ujumbe ule ule. Kimya kimya, basi mwangalie.

89 Wakati Petro alipomjia baada ya huduma Yake, Yohana Mtakatifu 1. Petro alimwendea. Hakuwa anaitwa Petro wakati huo; alikuwa anaitwa kwa jina lingine. Na wakati alipomwendea, Yeye alisema, "Wewe ni Simoni, na baba yako ni Yona."

Mzee huyo mvuvi aliwaza, "Yeye alinijuaje?"

90 Halafu Filipo, kutoka Bethsaida, pia, anapanda kuzunguka mlima, ndipo akampata rafiki fulani, Nathanaeli, chini ya mti, anaomba. Akasema, "Njoo, uone yeye ambaye tumemwona: Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu."

Angalia sasa jinsi alivyojifunua.

91 Naye akasema, "Je! laweza neno jema kutoka Nazareti?"

92 Akasema, "Njoo uone." Hilo ndilo jibu zuri sana mtu ye yote analoweza kutoa. Usilikosoe. Njoo, ujionee mwenyewe. Loo, laiti tungalikuwa waaminifu namna hiyo, leo.

93 Na katika safari yake, akaanza kumfundisha. Mbona, alisema, "Petro, jana, mtu fulani . . . Kefa, je! unamjua yule mzee mvuvi?"

"Ndiyo."

94 "Yeye alienda mbele ya Mtu huyu, naye akamwambia kwamba alikuwa nani na kwamba baba yake alikuwa ni nani."

"A-ha," kasema, "Nathanaeli, sijui kuhusu jambo hilo."

95 Na wakati alipoenda mahali Yesu alipokuwa, kwenye mstari ambapo alikuwa akiwaombea wagonjwa, Yesu alimkazia hayo macho, na kusema, "Tazama, Mwisraeli ambaye ndani yake hamna hila."

96 Yeye alijuaje alikuwa ni Mwisraeli? Wayunani na kadhalika, walivalia nguo sawa na walifanana. Yeye alijuaje kwamba alikuwa ni Mwisraeli? Alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Yeye alifanya nini? Aliangalia na akamwona.

Akasema, "Ulinijua lini, Rabi?"

97 Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, wakati ulipokuwa chini ya ule mti, nilikuona."

98 Akasema, "Hilo linatosha. Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli."

99 Yesu akasema, "Kwa sababu nimekwambia jambo hilo, unaamini?" Kasema, "Basi unaweza kuona mambo makubwa kuliko hili."

100 Lakini mfuasi wa kanisa asiyeamini alisimama hapo karibu. Loo, mwenye kicho na mwaminifu wawezavyo kuwa. Hakika. Walikuwa wamesimama pale wakiwa na elimu kubwa, ujuzi mwingi sana wa theolojia za seminari. Wakasema, "Mtu huyu ni mpiga ramli. Yeye ni Beelzebuli."

101 Yesu akasema, "Mnasema haya kwangu, nitawasamehe. Lakini wakati Roho Mtakatifu atakapokuja na kufanya jambo lile lile, neno moja dhidi Yake halitasamehewa, katika ulimwengu huu wala hata katika ulimwengu ujao."

102 Kulikuwako na mwanamke mdogo kutokwa na damu. Naye akapitia kwenye umati wa watu na akagusa vazi Lake, kwa kuwa

alisema kimoyomoyo, "Kama ninaweza kumgusa Mtu huyu, nitakuwa mzima." Akamgusa. Akakimbia na kujichomeka ndani ya umati huo wa watu, akaketi chini, ama cho chote alichofanya.

Ndipo Yesu akageuka, akasema, "Ni nani aliyenigusa?"

103 Petro akamkemea. Akasema, "Angalia, umati wote unakugusa. Kwa nini unasema, 'Ni nani aliyenigusa?'"

104 Akasema, "Lakini nimekuwa dhaifu. Nguvu, ama uweza, umenitoka." Ndipo akaangalia kote, kwa macho hayo, mpaka akampata. Yeye alifanyaje jambo hilo? Hilo hatujui. Bali ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Naye akajifunua kwa taifa la Kiyahudi kwa njia hiyo.

105 Wakati alipokuja kwa Wasamaria, huyo mwanamke alikuwa pale kisimani, mwanamke mzuri Msamaria.

106 Kumbukeni, kuna mataifa matatu tu ya watu. Hayo ni, Myahudi, Mmataifa, na Msamaria; watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Naye Msamaria alikuwa ni nusu Myahudi na nusu Mmataifa. Nanyi mnakumbuka wakati jambo hilo lilipoanza, ni wakati walipowaoa wake zao, na kadhalika.

107 Ndipo mwanamke huyu kijana akaja pale, ambaye tunaamini katika nchi yetu kwamba ni mwanamke mwenye sifa mbaya, bali hakuwa hivyo. Mvulana huyu kutoka huko India angewaambia jambo hilo. Hiki ni Kitabu cha mashariki, nanyi mnajaribu kukisoma kwa elimu ya magharibi.

108 Nilipoenda India, na nikashuka toka kwenye—kwenye ndege, huko Bombay, kulikuwako na askofu wa kanisa la Kimethodisti, na hao wote, wamesimama pale. Kasema, "Usitwambie ya kwamba wewe ni mmishenari, Bw. Branham. Tunajua zaidi juu ya Biblia kuliko ninyi Wamarekani mtakavyopata kujua." Na hiyo ni kweli. Akasema, "Sisi tulikuwa na Biblia kwa muda wa miaka elfu mbili kabla hamjakuwa taifa." Hiyo ni kweli. Kanisa la Mtakatifu Tomaso lingaliko kule, ambako Mtakatifu Tomaso alishuka akaenda kuhubiri. "Lakini," alisema, "tunasikia ya kwamba Mungu amewazuru, apate kuifanya Biblia hii kuwa hai tena." Kasema, "Hilo ndilo tunalotaka kujua." Ndivyo hivyo. Ulimwengu una njaa ya mkate ulio hai.

109 Mwanamke huyu Msamaria, alipokuwa amesimama pale kisimani, Yesu alimwambia, "Mama, nipe maji ninywe."

110 Vema, akasema walikuwa na ubaguzi. Lakini Yeye akamfahamisha ya kwamba hakukuwako na tofauti yo yote. Mungu aliwaumba, kwa damu moja, watu wote.

111 Ndipo akasema, "Kama ungalijua ni Nani ulikuwa ukizungumza naye, ungeniomba nikupe maji unywe."

112 Ndipo mazungumzo yakaendelea mpaka akaipata roho yake. Ndipo akajua shida yake ilikuwa ni nini. Akasema, "Nenda ukamwite mumeo na mje hapa."

113 Ilikuwaje wakati yule Myahudi alipoambiwa jambo hilo? Myahudi alisema, "Wewe ni Mwana wa Mungu." Hiyo ni kweli.

114 Ilikuwaje kwa mwanamke Msamaria wakati alipoambiwa jambo hilo, aliposema, "Nenda kamwite mumeo na mje hapa."

115 Alisema, "Bwana, ninaona ya kwamba Wewe u nabii. Sasa, tunajua ya kwamba Masihi ajapo, ambaye anaitwa Kristo, atakapokuja, Yeye atatwambia mambo haya. Lakini wewe u nani?"

Akasema, "Mimi ninayesema nawe ndiye."

116 Akakimbia mjini, naye akasema, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimetenda. Je! haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?"

117 Wala hakufanya hivyo kamwe, wakati mmoja, kwa Mmataifa. Kwa nini? Yeye aliliacha mpaka kwenye siku hii. Hivyo ndivyo alivyosema hapa, "Katika siku ambayo Mwana wa Adamu atajifunua Mwenyewe kutoka Mbinguni." Yeye anajifunua sasa, kwa Kanisa, kwa ajili ya rehema. Mara nyingine atakapojifunua, ni katika maangamizi, kwa hao ambao wameukataa Ujumbe.

118 Mungu aturehemu kwa. . .kwetu sisi, tunapoomba kwa muda mfupi. *Kwa Upole Na Kwa Huruma*, Dada Gertie, tafadhali.

119 Ninashangaa tu, usiku wa leo, nikiwasikitikia ninyi mliosimama kwenye kuta. Nami ninaweza kuhisi matarajio yenu. Ninashangaa tu, loo, kama mtakuwa waaminifu kwenu wenyewe na kwa Mungu, kwa muda kidogo tu.

120 Je! kweli mnataka kuharakisha na kutoka kwenye jambo hili? Kuna Mtu aliyepo usiku wa leo, anayeitwa Bwana Yesu. Yeye ana tikiti yako, na yote unayopaswa kufanya ni kumpa tu moyo wako. Yeye atauosha katika Damu Yake Mwenyewe, na kukusafisha na dhambi yote na mashaka, naye atakupeleka katika Mbinguni Yake waakati atakapokuja.

121 Na huenda jambo hilo likatukia kabla ya asubuhi, hayo masputniki. Hakuna jambo hata moja ambalo sayansi inasema. . .Mnalisikia, kila siku, kwenye redio, wakati wakiwa kwenye televisheni, wakati wanapowahoji hawa wanasayansi. Wao wanasema, "Hakuna kitu cha kuzuia ulimwengu huu usilipuliwe dakika yo yote." Inahitaji tu kunywa pombe ya Vodka kiasi cha kutosha, nao watafyatua wenzo fulani, na yote yamekwisha.

122 Hima! Ujumbe ni wa haraka. Hima! Ujisalimishe! Kimbia ukayaponye maisha yako! Toka humo. Toko kwenye Babeli hii ya kisasa. Ondokeni kwenye kuta hizo. Je! huwezi kusikia kitu fulani kikiuvuta moyo wako? Kama wewe kweli ni wa kiroho, na Mungu ananena nawe! Hakika, kama Yeye alinena na wale ndege wadogo, anaweza kunena nawe.

123 Je! unaweza kumwinulia mkono? Hatuna nafasi ya kuwaita watu kuja madhabahuni. Lakini kama tu utainua mkono wako, na kusema, "Mungu, unirehemu." Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki. Loo, jamani! Kote jengoni. Sijui kuna mikono mingapi. "Unirehemu, Ee Mungu. Huu ni mkono wangu. Ninataka kujiponya, Bwana. Kabla ya asubuhi, huenda nikasikia mayowe, niangalie huko nje na pinde za mvua zitakuwa zikielea mbinguni, Mwana wa Adamu atakuwa anakuja."

124 Ni siku ya kutisha jinsi gani, ambapo ulipoteza nafasi yako. Ulisimama kabisa kanisani mwako, sivyo? "Loo," ukasema, "mama yangu alikuwa mfuasi wa hili." Hiyo ni kweli, ndugu. Hilo ni sawa, dada. Lakini wokovu wa mama kamwe hautakuingiza ndani. Mama aliishi katika siku moja, nawe unaishi nyingine.

125 Usikie Ujumbe wa Bwana, na sikia onyo la Roho. Ilikuwa ni Roho ya aina gani, Yule aliyetambua jinsi Sara alivyokuwa anacheka ndani ya hema? Malaika wa Bwana.

126 Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, ninataka kumwombea kila mmoja wenu.

127 Ulifanya nini wakati ulipoinua mikono yako? Unasema, "Hilo lilimaanisha lo lote, Ndugu Branham?" Hakika lilimaanisha. Kama kweli ulimaanisha jambo hilo, lilimaanisha tofauti kati ya mauti na Uzima. Ujumbe ni wa haraka sana. Mbona usiinue mkono wako juu sasa hivi? "Mungu, nirehemu."

128 Mungu ambariki yule msichana mdogo. Mungu ambariki huyo bibi. Mungu akubariki; wewe, mwanangu; wewe, wewe, kijana mwanamume. Watoto wadogo kote kote hapa madhabahuni wameinua mikono yao juu. Vema, nawatakia heri!

Unasema, "Hawamaanishi jambo hilo." Loo, ndiyo, wanalimaanisha.

129 Yesu alisema, "Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, msiwazuie, kwa kuwa watoto kama hao ufalme wa Mungu ni wao." Huenda wasiishi wakawa watu wazima. Lakini, watakuwa hivyo. Hawataninii kabisa . . . Watajiponya, labda, na mambo yote makuu ambayo imetulazimu kupitia.

130 "Mungu, turehemu!" Wakati unapoinua mikono yako, inaonyesha ya kwamba kuna kitu fulani ndani yako ambacho kimeamua. Mwili wako ungekuwa umekufa kama kusingekuwako na kitu fulani ndani yako, ambacho kilisema, "Inua mikono yako." Huyo alikuwa ni Roho. Ndipo unainua mkono wako. Mungu alishuhudia jambo hilo. Roho alikufanya uinue mikono yako.

131 Mungu akubariki, na watoto wote wadogo kule nyuma. Watoto hao wadogo weusi, pia, kule, Mungu aibariki maskini mioyo yenu midogo, kipenzi. Mungu anakupenda. Hakika.

132 Tutaondoka hapa, moja ya siku hizi. Sijui itakuwa ni lini, lakini ina—inakuja. Hima, upesi sana, ingieni kwenye ufalme! Unasema, "Vema, nimesikia jambo hilo hapo awali." Huenda ukalisikia kwa mara yako ya mwisho, pia. Hebu huu uwe ndio huo wakati.

Mungu akubariki huko nyuma, wewe msichana.

133 Ondokeni kwenye upuuzi huu wa kisasa uliooza, kuta hizi za kale. Zote zitaanguka. Hizi roki hizi zote na upuuzi huu wote vitaangamia pamoja na ulimwengu. Usihesabiwe pamoja na ulimwengu. Ondokeni humo. Mungu anakuja kwa ajili ya Kanisa Lake. Yeye amekuchagua, hiyo ndyo sababu anazungumza nawe. Ujumbe ni wa haraka. Njoo upesi!

134 Sasa, wakati tukiomba, uwe mwaminifu sasa na umwombe Mungu akurehemu.

135 Bwana uliyebarikiwa, huenda kukawa na watu hapa ambao hawajaona kabisa matendo ya nguvu za Mungu maishani mwao, lakini kitu fulani ndani ya mioyo yao kimesema, "Inua mkono wako. Ni Mimi." Nao wanaona ya kwamba kuna wito wa haraka sana. Wao, wao ni watu wenye akili vya kutosha kuangalia kila mahali na kuona ya kwamba kuna jambo fulani linalokaribia kutukia.

136 Watoto wadogo, wengi wao waliinua mikono yao midogo. Mungu, warehemu. Wengi wa wazee na wa umri wa makamu, waliinua mikono yao. Matineja waliinua mikono yao. Wanataka rehema, Mungu. Nami ninafurahi sana kujua ya kwamba ufunuo wa kwanza wa Kristo ni rehema; ufunuo wa pili ni hukumu. Ee Mungu, tunashukuru kwa ajili ya hawa ambao wamechukua rehema usiku wa leo, njia ya rehema. "Heri wenye rehema, kwa maana watapata rehema. Heri wenye njaa na kiu ya haki; watashiba."

137 Washa taa zao, usiku wa leo, Bwana. Jalia wawe taa zilizowekwa juu ya kilima, ambazo haziwezi kufichwa, bali zinatoa mwangaza katika mashule na mahali ambako zitaunganishwa, tangu sasa. Tujalie, Bwana. Jalia wawe taa zitakazowaka kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Wabariki.

138 Na katika siku fulani, katika ulimwengu ulio bora zaidi, Bwana, jalia sote tukusanyike kuizunguka ile meza kuu ya Mungu, kwenye Karamu ya Arusi. Dumisha Roho Yako juu yetu, Bwana. Wabariki wale wanaosimama karibu na kuta, na nje huko kwenye ukumbi na kila mahali, walioinua mikono yao, na kadhalika. Uwe pamoja nao, Bwana. Wamesimama, na maumivu ya viungo, usiku wa leo. Lakini, uturehemu. Tujalie mambo haya.

139 Wao ni matunda ya Ujumbe huu ulioharakishwa usiku wa leo. Naomba ya kwamba malaika wa Bwana watalifanya halisi sana mioyoni mwao, hivi kwamba hawata—hawatakosa lo lote la Hayo. Nao ni matunda, nami ninawakabidhi Kwako. Nawe uwatoe kwa Yesu, kwa maana hao ni zawadi Zako za upendo Kwake. "Hakuna mtu anayeweza kuwapokonya kutoka katika mkono huo, maana hakuna aliye mkubwa kuliko Mungu." Nami ninaomba ya kwamba Wewe utawaweka salama salimini mpaka Yesu atakapokuja kuwachukua.

140 Jalia hao wengine wafanye haraka, Bwana, na kuharakisha, kwa kuwa Ujumbe huu ni wa haraka sana. Inatubidi kutoka haraka kabla maangamizi hayajaja. Na sasa, Bwana Mungu, ninaomba ya kwamba utamtuma Malaika wako, yeye yule aliyeketi pamoja na Ibrahimu. Tujalie, Bwana. Naye aliweza kujua yale Sara aliyokuwa akifanya, huko nyuma hemani. Na huyo alikuwa ni yule Malaika wa Agano. Huyo alikuwa ni yule Malaika aliyeleta rehema kabla moto haujashuka. Karibu wakati wo wote, moto ungeweza kushuka sasa, atomi ambazo zingeuvunja ulimwengu mzima vipande viwili. Nasihi aje usiku wa leo na atupe rehema, Bwana, kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

141 Loo, kuna kitu fulani kuhusu Injili ya kale iliyobarikiwa, inaonekana kana kwamba inasugua kabisa kabisa. Ninaipenda.

142 Hebu na tuimbe tu huo mara moja, "Kwa upole na kwa huruma Yesu akuita." Kila mtu, hebu tu na tumwinulie mikono yetu. Je! mtafanya hivyo?

> Kwa upendo na kwa huruma Yesu anakuita,
> Anakuita wewe na mimi,
> Ingawa tumetenda dhambi, Yeye ana huruma
> na msamaha,
> Msamaha kwako na kwangu
>
> Njoo nyumbani, njoo nyumbani, (Jifungie
> ndani tu pamoja na Kristo sasa.)
> Ninyi mliochoka, njoni nyumbani;
> Kwa bidii, kwa huruma, Yesu anakuita,
> Anakuita, Ee mwenye dhambi, uje nyumbani!

143 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . hujawahi kuwa kwenye moja ya ibada zetu za uponyaji, hebu tuone mikono yenu. Hujawahi kuwa kwenye ibada hizo? Sawa. Ninafurahi kuwa pamoja nanyi hapa.

144 Sasa, sidai kuwa mponyaji. Ninadai ya kwamba Yesu hajafa, bali yu hai. Mimi si mponyaji. Hakuna waponyaji. Kristo amekuponya tayari. "Kwa mapigo Yake uliponywa."

145 Lakini ninataka kuwauliza ninyi wageni jambo fulani. Sasa, labda mnaenda kwenye kanisa fulani. Wengi wenu mliinua mkono wenu hivi punde tu, uliinua mkono wako kwa ajili ya maombi, kitambo kidogo kilichopita. Kama

huna kanisa ulilochagua, tunakukaribisha katika Maskani ya Branham hapa, ambapo Ndugu yetu mpenzi Orman Neville, mtu mcha Mungu anayefundisha kweli tupu, kutoka katika Biblia. Mnakaribishwa kwenye ushirika wetu. Tunaninii tu . . . Si madhehebu. Sisi ni kanisa tu hapa, ushirika. Sisi ni Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Pentekoste, Lutheri, tuko yote. Sisi ni Wakristo wanaowapenda ninyi. Nasi tunaomba ya kwamba utajipatia . . . Kama huwezi kuja hapa, jitafutie kanisa zuri la nyumbani, mahali fulani, ambako kweli wanahubiri Injili, na ili kwamba upate kulishwa na Roho wa Mungu.

146 Kila mahali, kote jengoni, usiku wa leo . . . Kama Bwana Yesu amefufuka kutoka katika wafu, nami nimewaambia Kweli, basi Mungu anawajibika kwa Neno Lake, kulidhihirisha. Unaona?

147 Loo, usiogope kulitumainia. Hilo aidha ni Biblia, ni Kweli, ama si Kweli. Kama si Kweli, ni danganyifu sana kuliko yote iliyowahi kuandikwa, kwa maana imewadanganya mamilioni. Nimesimama, mara nyingi, nikiwa nimeshika Kurani katika mkono mmoja na Biblia katika huo mwingine, mbele ya Waisilamu, na kusema, "Kimoja ni cha kweli na kingine ni cha uongo. Hebu Mungu, ambaye ni Mungu halisi, anene." Usiogope. Yeye hatakupungukia kamwe. Hatakuacha kamwe.

148 Sasa, Bwana Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, kazi alizozifanya, ambazo ndiyo kwanza tuzinukuu, Yeye aliahidi ya kwamba atakuja tena kabla ya wakati wa mwisho na angefanya mambo yale yale. Alisema angeyafanya hayo kupitia Kanisa Lake. Sasa, Yeye alisema, "Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi." Sasa, Mzabibu hauzai tunda. Matawi ndiyo yanayozaa tunda.

149 Sasa, kama ni tawi la boga, litazaa maboga. Kama ni tawi la tikiti maji, litazaa matikiti maji. Kama ni tawi la tango, litazaa matango. Kama ni tawi la mzabibu, litazaa zabibu.

150 Kama ni tawi la Kikristo, litamzaa Kristo, Uhai wa Kristo, kazi za Kristo. Unaona? Ndipo, roho zetu hazina budi kutiwa nguvu na kitu fulani.

151 Ninafurahi sana kuwa ndani Yake, usiku wa leo. Hamjui, enyi kundi dogo, jinsi linavyonifanya kujisikia, kujua hapa, nina umri wa miaka arobaini na nane, ni mzee. Na nimehubiri sasa kwa muda wa miaka ishirini na saba. Mabega yangu yanainama. Na, loo, ninatambua mimi si mvulana huyo mdogo aliyekuwa akicheza gololi nje hapa mtaani. Lakini kuna jambo moja ninalojua, mimi ni mtumishi Wake. Afadhali nipate hilo kuliko yote nijuayo. Kwa maana kitu kingine cho chote kitafaa nini?

152 Nimejaribu kuwa mwaminifu kwenu ninyi watu. Nimejaribu kufanya kila kitu nilichoweza kufanya ili nipate kuwa mwaminifu na mwenye haki na mkweli, mbele zenu na mbele za Mungu, kwa maana ninajua Yeye anatuangalia wakati wote. Sasa, kama ningeweza . . .

153 Nitawaambia sasa. Ujumbe huu mdogo usiku wa leo, nilijaribu kuumaliza mapema, bali ninaomba ya kwamba Mungu atachukua yale yaliyosalia na kuyaweka moyoni mwenu. Hima! Hima! Hima! Tokeni Babeli, upesi mwezavyo. Msikae ulimwenguni. Ondokeni kwenye upuuzi huo. Njoni huku, mkawe huru, pamoja na Kristo. Ondokeni kwenye mambo hayo. Kwa kuwa hamjui ni saa gani ambapo huenda kusiwe na kitu ila vumbi tu lililosalia juu ya dunia hii, gesi tu, na ulimwengu huu wa kale umekwisha lipuliwa vipande-vipande. Linaweza kutukia kabla ibada hii haijaisha, wala jambo hilo lisingepingana na Maandiko hata kidogo. Lingetimiza tu Maandiko. Injili imekwisha kuhubiriwa. Huu hapa Ujumbe wa mwisho.

154 Sasa, msitarajie mambo makuu ya usoni. Marekani imekwisha tenda dhambi na kumaliza siku yake ya neema. Hiyo ni kweli kabisa. Andikeni jambo hilo kwenye Biblia zenu mwone kama niko sahihi ama nimekosea. Imekuwa ikishuka sasa kwa miaka miwili.

155 Billy Graham alisema, kwenye kiamshakinywa chake si muda mrefu uliopita. Aliinua Biblia juu. Akasema, "*Hiki* hapa ndicho kipimo. Paulo alienda katika mji fulani na akapata mwongofu mmoja, akarudi mwaka uliofuata na kulikuwa na thelathini." Kasema, "Mimi ninaenda katika mji na kuwa na ufufuo, wa waongofu elfu ishirini, kisha ninarudi katika muda wa miezi sita wala siwezi kupata labda ishirini."

156 Kuna nini? Kuna kiasi fulani tu cha samaki kwenye kidimbwi. Kuna kiasi kadha tu ambacho Mungu alijua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na wamechaguliwa tangu zamani kwa ajili ya Uzima wa Milele. Wakati huyo wa mwisho atakapoingia, mambo yamekwisha.

157 Kulikuwa na na kiasi fulani tu cha ndege kilichoingia safinani, kiasi fulani tu cha wanyama mbalimbali kilichoingia kwenye safina ile. Na mlango ukafungwa, na Mungu, na hao wengine wakaachwa nje, ingawa walijaribu kuingia.

158 Na rafiki yangu mpendwa, kama wewe hauko ndani, ingia ndani sasa hivi, wakati Mungu angali anaita, maana milango ya rehema huenda ikafungwa, kwa Mmataifa, wakati wo wote. Sasa, na sasa jambo ninalofanya, sasa, litakuwa . . . Yale nitakayosema sasa . . .

159 Nimenena, na maneno yangu, kama nilikuwa nimehubiri kwa muda wa saa kadha, haingekuwa na nusu faida ya neno moja kutoka kwa Kristo wetu anayestahili kuabudiwa. Sasa, lakini yale niliyohubiri, ama nimesema Kweli ama ni uongo. Kama nimesema uongo, Mungu hatahusika nao. Kama nimesema Kweli, Mungu atasimama nyuma ya Neno Lake.

Unasema ni ngapi? Ati uligawa kadi hamsini?

160 Nitawaonyesha ni kwa nini inatubidi kugawa kadi, wakati unapokuwa na mkutano wa utambuzi. Mimi sisemi ya kwamba Yeye atafanya jambo hilo. Huenda asilifanye. Lakini ninawatakeni mwe waaminifu kwangu. Ni wangapi walio hapa ndani wangetaka kuja mstarini sasa? Inueni mikono yenu, kila mahali humu jengoni, po pote ulipo. Kila mtu humu jengoni anayetaka kuja mstarini, inueni mikono yenu. Sasa ungeninii vipi. . . Ni nani angetaka kuwa wa kwanza? Unaona? Usingeweza kufanya jambo hilo. Inatubidi kugawa kadi, kusudi tudumishe m—mstari.

161 Sasa, yeye amegawa kadi hamsini. Na hebu na tuite kutoka kila upande, kwa kutumia bunda hilo la kadi, na hiyo itampa kila mtu nafasi ya kuja.

162 Sasa, si yale yanayotendeka *hapa*. Ni yale yanayotendeka *hapa*. Unaona? Si ninii, niguse. Ni, kumgusa Yeye. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Agano Jipya, Kitabu cha Waebrania, kilisema ya kwamba sasa hivi, ya kwamba, "Kristo ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuliana nasi katika mambo ya udhaifu wetu."? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, ungewezaje kujua ya kwamba ulimgusa? Kwa, Yeye anakujibu moja kwa moja, kama tu alivyofanya. Kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, inambidi kujidhihirisha vile vile kama alivyofanya jana na milele. Kwa hiyo, unaona, ujumbe wa mwisho kwa Wayahudi na hao wengine, alifanyaje jambo hilo? Sasa hii ndiyo ninii ya mwi-. . .

163 Kama alijidhihirisha kwa njia nyingine yo yote, kupitia kwa madhehebu fulani, angekuwa asiye na haki. Yeye hakujidhihirisha hata kidogo katika madhehebu fulani, kwa maana hakukuwako na madhehebu katika siku Zake. Alijidhihirisha kwa miujiza, kama tulivyosema asubuhi ya leo, kama vile yale maandiko ya mkono kwenye ukuta, ile tafsiri. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mungu awe pamoja nanyi sasa.

164 Alisema, "Moja hadi hamsini." Vema. Ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja, tafadhali inua mkono wako. Angalieni kadi zenu. Mtu fulani kwenye machela, ama po pote pale, na hawezi kusimama, kila mtu aangalie kadi ya mwingine. Ni kadi ndogo tu. Hata sidhani hizi zina picha yangu. Ni kadi ndogo tu isiyo kitu. Namba moja, po pote ulipo. [Mtu fulani anasema, "Iko hapa."—Mh.] Vema. Tafadhali simama tu mahali ulipo, bwana. Namba mbili, tafadhali inua mkono wako. Huyu bibi papa *hapa*. Namba tatu, tafadhali inua mkono wako. [Sehemu tupu kwenye kanda.]

165 Sisi hatufahamiani. Huu ni wakati wetu wa kwanza kukutana basi, maishani, nadhani. Basi, Bwana Mungu anatujua sisi wote wawili. Anajua yote kukuhusu, na anajua yote

kunihusu mimi. Lakini kama Yeye, katika wema Wake, angeweza . . .

166 Kama ningekwambia, “Loo, bwana, wewe ni mgonjwa. Nami . . . Utakuwa mzima.” Ungekuwa na haki ya kushuku jambo hilo. Wasikilizaji hao wana haki ya kuduwazwa na jambo hilo. Bila shaka. Ulipata neno langu tu.

167 Lakini kama Roho Mtakatifu atakuja na kumwambia mtu jambo fulani ambalo ametenda, jambo ambalo mimi sijui neno juu yake, ambalo limekwisha tukia, huyo mtu atajua kama hilo ni kweli ama si kweli.

168 Basi kama Yeye anajua yaliyokuwako, hakika, kama hilo ni kweli, Yeye anaweza kukwambia yatakayotukia, na itakuwa ni kweli.

169 Unapaswa kuamini jambo hilo, Bibi Cox, sivyo? Bibi Cox anayeketi pale, ilitokea tu kwamba nilimwona, anatoka Kentucky, kutoka hapa. Huyo ni Bibi Wood . . . hapa mahali fulani kanisani, mama yake. Kansa ilikuwa tayari imeula uso wake kabisa, *hapa* ndani.

170 Nilikuwa nikija kutoka kwenye misitu ya kaskazini. Mke wangu alinipigia simu, akasema, “Sijapata kuona mtu ye yote aliyefadhaika namna hiyo maishani mwangu, kama—kama Bibi Woods.” Na Bw. na Bibi Woods ni rafiki wangu wasiri. Basi nikamwendea huyo bibi, nikarudi nikiwa na BWANA ASEMA HIVI. Hiyo kansa ikafa.

171 Pale, mwanamke huyo ameketi pale, na ni vigumu kwako kujua ni nini . . . Tafadhali inuka tu, Bibi Cox, ili kwamba watu waweze kukuona. Upande wote mzima wa pua yake na kadhalika, ulililiwa na kansa, mpaka kwenye macho yake. Geuka ili wasikilizaji waweze kukuona kule nyuma. Kansa.

Yeye ni sahihi daima. Hakosei kamwe.

172 Sasa, kama Bwana Mungu wetu atamfunulia ndugu huyu, na awe hakimu, kama Bwana Mungu atamfunulia kilichomleta hapa. Ama, kitu kama alichomfanyia yule mwanamke kwenye . . . Ama, kama ambavyo angesema alimfanyia Filipo, wakati Nathanaeli alipomwona Yeye . . . ama Nathan- . . . Filipo alipomwona Nathanali. Na atafunua jambo hilo; je! ninyi nyote mngeamini, ninyi wote mtaamini? Kama—kama mtu huyo anajua mimi sijui lo lote juu yake; nami nimeinua mikono yangu, sijui jambo lo lote juu yake. Aliinua mkono wake, ya kwamba sikumjua, ama yeye hanijui. Basi kama Bwana atafunua jambo hilo, ninyi nyote mtalikubali, sivyo? Ni wangapi? Inueni mikono yenu ili niweze tu kuona. Sasa Bwana awabariki.

173 Sasa, bwana, ninasimama hapa tu, nikingojea kuona yale atakayoniambia, kwa hiyo ninyi mwe waamuzi. Na kama mtu ye yote anaweza kuangalia, mtu huyu amefunga macho yake, kwa hiyo mnaona haingeweza kuwa ni telepathia. Endelea

tu kufunga macho yako. Kama Bwana wetu Yesu. . .Kama atafunua jambo hilo, tutamshukuru.

174 Lakini mtu anayesimama mbele yangu, kitu kilichomleta hapa, ni jambo la kiroho analotaka liombewe. Hiyo ni kweli. [Mtu huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako ili watu waweze kuona. Sasa unaamini? Sijapata kumwona maishani mwangu, bali ilikuwa ni hilo. Jambo fulani linamsumbua akili. Sasa, kadiri ninavyoendelea kuzungumza naye, ndivyo mengi yangeweza kusemwa. Sasa iweni na kicho.

175 Yule Malaika yule alifanya nini? Alikuwa amempa kisogo, naye akasema, "Kwa nini Sara amecheka?"

Akasema, "Sikucheka."

Akasema, "Naam, ndiyo, ulicheka." Maana, aliogopa.

176 Sasa kama wasikilizaji wangali wanaweza kusikia sauti yangu, kwenye spika. Mtu huyu anaonekana akiondoka kutoka kwangu. Ninamwona mwanamke amesimama. Hilo ndilo jambo muhimu liliomleta mtu huyu hapa. Ni kwa ajili ya mke wake, naye hayuko hapa pamoja naye. Na ana shida ya kike, shida ya akina mama, naye anaumwa na mgongo wake. Hiyo ni kweli.

177 Hutoki katika mji huu. [Mtu huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Umetokea mji mwingine, unaoitwa Marysville. ["Hiyo ni kweli."] Hilo ni sawa. Sasa nenda nyumbani ukalikute jinsi ulivyoamini. Itakuwa namna hiyo, katika Jina la Bwana. Mungu akubariki. Leso hiyo, haitakulazimu kumwekea, ulikuwa nayo mfukoni kwa ajili yake, bali hutaihitaji.

178 Ninakujua. Sijui jina lako. Lakini wewe ni yule mwanamke aliyekuwa amesimama pale kwenye mlango wa nyuma, siku moja, ambapo Malaika wa Bwana alinijia, wakati ilipokuwa ni mara yako ya kwanza hapa maskanini, na kafunua jambo fulani lililokuwa ni siri kabisa. Nawe uliponywa, ugonjwa wa kansa. Hiyo ni kweli. [Huyo mwanamke anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Lakini sina fununu una shida gani sasa. Sijui. Unajua jambo hilo. Sina fununu una shida gani. Lakini, kama Bwana ataifunua, je! utalikubali? ["Ndiyo."] Mimi . . .

179 Wewe hauko hapa kwa ajili yako. Uko hapa kwa ajili ya mtoto fulani. Na mtoto huyo anateseka. [Mwanamke huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Na maumivu hayo yako kwenye uti wa mgongo. ["Ndiyo."] Ni kama kwamba, hawezi kusimama, ama kitu kama hicho. Nami nimewaona wazazi wa mtoto huyo, wakiwa na rosari. Wao ni Wakatoliki. ["Ndiyo."] Na mume na mke wazee, ni, babu zao ni Katoliki, pia. ["Ndiyo."] Nawe umesimama kwa niaba ya mtoto huyo. Chukua leso yako na uiweke juu yake. Usiwe na shaka, unaweza kupata ulichoomba. Sasa amini kwa moyo wako wote.

Unaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

180 Nadhani simjui mama huyu. Sisi hatufahamiani, bali Bwana Yesu anatujua sisi sote wawili. Sasa hapa pana picha kamilfu. Hii hapa picha ya Yohana Mtakatifu 4. Mwanamke mweusi, mwanamume mzungu; katika siku ile, ilikuwa ni Msamaria, na Myahudi, jamii mbili za watu. Yesu alimfahamisha, upesi, ya kwamba hakukuwako na tofauti. Sisi sote ni viumbe vya Mungu. Nchi tunayoishi, hubadilisha rangi yetu, haina uhusiano wo wote na jambo hilo. Mungu aliwataka watu Wake wawe hivyo. Alimfanya mtu kuwa mweupe, mweusi, hudhurungi, manjano, mwekundu. Aliwafanya hivyo. Hiyo ni kazi yake. Naye anatupenda sisi sote. Lakini hii hapa picha kamilifu, watu wawili ambao hawajapata kukutana hapo nyuma, na mara yetu ya kwanza, jamii mbili mbali mbali.

181 Sasa, ninaona ya kwamba wewe ni mwamini. Wewe ni Mkristo kwa sababu roho yako ni karimu. Na huyo Malaika mkuu wa Mungu asingekaribisha kitu cho chote ambacho kilikuwa ni kibaya. La, hasha. Unaona ile picha pale juu, yule Malaika kwenye ile picha pale, ile Nuru juu ya mahali pale ninaposimama? Huyo ndiye anayekufanya kujisikia jinsi unavyojisikia sasa. Yote inashuka tu juu yako.

Hebu kidogo, Dada Gertie.

182 Inaonekana kwamba ni kitu fulani, siwezi kumpata bibi huyo vizuri. Naam. Mwanamke huyu anaugua ugonjwa wa wasiwasi. Yeye hushikwa na wasiwasi. Anaangusha vitu. Hiyo ni kweli. Halafu una shida ya kiroho unayojaribu kuitatua, kwa maana umekuwa ukiiombea kwa muda mrefu. Hiyo ni kweli. Na una yabisi kavu. Ninakuona ukijaribu kuamka kutoka kitandani, pole pole, hasa sana asubuhi. Una kasoro fulani kwenye uti wako wa mgongo, pia, shida ya uti wa mgongo. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

183 Unaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu? Unaamini Mungu yeye yule aliyemjua Simoni angekujua wewe? Kama Mungu atafunua jambo hilo, je! litakufanya mwamini mwenye nguvu, kwamba utapata utakachopata? Wanakuita, "Nanny." [Huyo dada anasema, "Amina."—Mh.] Na jina lako la mwisho ni Johnson. ["Amina."] Nawe unaishi New Albany. Rudi nyumbani na uwe mzima, katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

Amini tu.

184 Je! tunafahamiana, ewe bibi? Ndiyo. Ili kwamba tu—ili kwamba tu watu waone, tafadhali inua mkono wako, useme, "Hatufahamiani. Ninii tu . . ." Sasa Bwana Mungu anatujua sisi sote wawili. Na kama Yeye atakujalia ombi hili, utalifurahia?

Sasa baadhi yenu mmeanza kuamini.

185 Sasa, mzungu fulani anaendelea kutokea mbele ya mwanamke huyu hapa.

186 Ni mtu huyo anayeketi papo hapo. Unaninii . . . Hiyo ni sawa, keti tu mahali ulipo. Una shida ya figo. Una shida ya mgongo. Na una shida ya tumbo. Hiyo ni kweli. Sasa nenda zako, ukiamini, wala haitakusumbua tena.

187 Aminini tu. Ninaitolea imani yenu changamoto. Ni wangapi mnaamini kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, basi tazameni mpate kuishi.

188 Kama Bwana Mungu wetu atamfunulia mwanamke huyu, ambaye ni mgeni kabisa kwangu. Na tumeinua mikono yetu juu, ya kwamba hatujakutana hapo awali, nijuavyo mimi. Na endapo Bwana Mungu wetu atamfunulia mwanamke huyu, na afanye jambo lile lile alilofanya, kama yule mwanamke kwenye ninii . . . Mwanamke Msamaria. Je! nyote mtaamini kwa moyo wenu wote, basi? Hilo litawaridhisheni kabisa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

189 Unaona, nina mkutano unaokuja. Sina budi kuondoka kesho. Nami sina budi kwenda huko Virginia, na kuna mkutano mkubwa unaokuja. Sitaki kujidhoofisha sana, kwa kusimama hapa. Vema, sitaharakisha, hebu kidogo, kuhusu mwanamke huyu. Nanyi aminini.

190 Kwamba mwanamke huyo ni nani, ana giza la kuchukiza linalomfuata. Loo, ni—ni huzuni. Umepatwa na shida fulani hivi karibuni. Ulipoteza mtoto, mtoto mchanga. [Huyo mwanamke anasema, "Ndio."—Mh.] Hiyo ni kweli. Na jambo lingine, unasumbuliwa na shida ya kike, shida ya akina mama, na shida ya mgongo. Na pia una namna fulani ya kitu fulani kinachotukia kwako, kama kuzimia. Loo, ni kifafa. Hiyo ni kweli. Wala hutoki katika mji huu. Ulivuka mto, kuja hapa. Umetoka Louisville. ["Ndiyo."] Unaishi kwenye namba, inayoitwa, Barabara ya 1754 ya West Oak. [Mwanamke analia kwa sauti kuu, "Ndiyo, ndiko ninakoishi."] Jina lako ni Margaret Quinn. ["Ndiyo."] Vema.

191 Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, mpe mwanamke huyu kile anachotamani, kwa kuwa ninamwamuru adui huyu amwache, katika Jina la Yesu. Amina.

192 Mungu akubariki, bibi. Usione shaka tena. Nenda na ukapokee sasa ulichoomba.

193 Mnaamini kwa mioyo yenu yote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

194 U hali gani, bwana? Hii ni mara yetu ya kwanza kukutana, nadhani. Je! unaamini Bwana Mungu wetu yuko hapa kukupa na kukutimizia haja zako? [Mtu huyo anasema, "Ndiyo, ninaamini. Ninajua Yeye yuko hapa. Ninaweza kumwona."—Mh.] Ninapenda ujasiri wako. Nawe uko hapa kwa jambo halali. ["Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli."] Unataka kuacha kunywa pombe na kuvuta sigara. ["Hiyo ni kweli."] Vema, imekuacha sasa. Nenda zako, na amani ya Mungu iwe pamoja nawe na kukufanya wewe uamini. Mungu awe pamoja nawe.

"Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana."

195 Unataka kuondolea mbali maumivu hayo ya mgongo? Shuka uende kule, ukimsifu Yeye, nawe utayaondoa. Nenda zako tu, ukiamini, kwa moyo wako wote.

196 "Kama unaweza kuanimi," Biblia ilisema. Iweni na kicho. Aminini yale Mungu anayofanya kuwa ni Kweli.

197 Ninakufahamu. Nitakuombea tu. Ninajua shida yako.

198 Bwana Mungu, mrehemu mwanamke huyu na umjalie ombi hili, kwa kuwa ninaomba katika Jina la Yesu. Amina. Sikumbuki. . .Je! jina lako ni Baker? [Huyo dada anasema, "Ndiyo, bwana."—Mh.] Hiyo ni kweli. Na—nakumbuka sasa. Mungu akubariki. Enenda moja kwa moja na umwamini kwa moyo wako wote. Vema.

199 Sikujui, bibi. Sisi ni wageni. Hiyo ni kweli. Je! unataka kula chakula chako cha jioni, uondolee mbali shida hiyo ya tumbo, hicho kidonda cha tumbo ambacho umekuwa nacho wakati huu wote? Nenda, ukale, basi, na Yesu Kristo akufanye mzima.

200 Ninakujua. Na ninajua kwamba shida yako ni gani. Hujui—hujui ya kwamba ninajua hilo, bali, ni—ninajua. Basi kwa kuwa umekuja hapa maskanini, sitaisema. Bali yabisi kavu zitakuacha kama tu utaamini. Enenda zako. Mungu akubariki.

201 Hebu na tuseme, "Asante Mungu." [Kusanyiko linasema, "Asante Mungu."—Mh.]

202 Wewe una wasiwasi, pia. Una shida ya tumbo linalokusumbua. Je! unaamini ya kwamba Bwana Yesu atakuponya? [Huyo dada anasema, "Ninaamini."—Mh.] Basi enenda zako, na amani ya Mungu na iwe juu yako. Ninataka tu kukuwekea mikono, nasi tuamini kwa mioyo yetu yote, ya kwamba Mungu atafanya jambo hilo.

203 Mimi ni mgeni kwako, nadhani, ewe bibi. Unanijua? Unahudhuria kanisa hili? Unahudhuria. Sijawahi kukuona. Bila shaka, watu wengi sana wanakuja. Vema. enenda zako, ukiamini, na shida hiyo ya kike itakuacha, shida ya akina mama uliyokuwa nayo. Unaamini? [Bibi huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Vema, basi nenda zako, na Mungu atakuwa pamoja nawe na kukusaidia, nina hakika.

204 Je! unaamini, bwana? Unaamini ya kwamba Bwana atakuondolea huko kukakamaa, na kukufanya mzima, hiyo yabisi kavu? Rudi moja kwa moja kupitia pale, ukimshukuru na kumsifu kwa ajili ya jambo hilo, ndipo utakuwa mzima.

205 Unasumbuliwa na ugonjwa wa wasiwasi, sivyo, bibi? Huo ni wasiwasi wa akili. Unakuwa mdhaifu sana, unapoteza fahamu, hasa sana alasiri. Hata Shetani amekwambia utakuwa kichaa. Hiyo ni kweli. Lakini ni uongo. Utakuwa mzima. Si kitu cho chote ila tu ni wakati wa maisha ambao unaingia. Ni wakati wa kukoma hedhi. Kila mwanamke hana budi kufikia hali hiyo.

Lakini utakuwa mzima sasa hivi. Je! unaamini neno langu? Basi nenda zako, mshukuru Mungu, na uimbe nyimbo na ushangilie, na uwe mzima.

206 Vema, dada. Mimi sikujui, pia. Jambo la ajabu, nilipomwambia jambo hilo, kitu hicho kilikuacha wakati uo huo, maana hiyo ndiyo iliyokuwa shida yako hasa, wasiwasi. Sasa enenda zako, na uamini kwa moyo wako wote, nawe utakuwa mzima. Amina. Nenda na uamini kwa moyo wako wote.

207 Ninakujua, ewe bibi. Ninakutambua kwa sura, lakini sininii . . . Unaamini Mungu atakuponya? Ninajua wewe u nani sasa. Wewe ni yule mama anayekuja hapa maskanini. Unaamini Mungu atakuponya? Hebu nikuombee tu.

208 Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, mpe mwanamke huyu afya, naomba, katika Jina la Yesu. Amina.

209 Usitie shaka. Siwezi kukumbuka jina la mwanamke huyu, lakini ninajua kwamba yeye ni . . .

210 Vipi kuhusu ninyi watu huko katika wasikilizaji? Je! mnaamini? Sasa ketini kimya kabisa. Iweni na uchaji sana. Upande huu *hapa*, mtu fulani. Ninaisai imani yako, katika Jina Jina la Yesu Kristo, kuamini jambo hili.

211 Bibi mweusi ameinua mikono yake juu, pale. Je! unaamini, ewe bibi, kwamba mimi ni mtumishi wa Mungu? [Mwanamke huyo anasema, "Ndiyo, bwana."—Mh.] Kama Mungu atanifunulia shida yako ni nini, je! utakubali jambo hilo? ["Ndio, bwana."] Wewe unataka kuombewa pamoja na yule msichana mdogo. Kwa ajili ya macho yako, unapoketi hapo. Hiyo ni kweli. Weka mkono wako juu ya mtoto yule, na uamini kwa moyo wako wote.

212 Bwana Mungu, ninaomba ya kwamba watapokea hili, katika Jina la Yesu. Amina.

Je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

213 Yule pale Malaika wa Bwana amesimama karibu na huyu jamaa mwenye nywele nyeusi. Ni—ninaamini yeye anahudhuria hapa kanisani, hata hivyo. Sina hakika. Bwana, endapo ninakujua, sijui una shida gani, isipokuwa Mungu anifunulie. Lakini ni rehema Zake zimesimama hapa. Nawe una ki—kidonda mguuni, mguu wa kushoto. Hiyo ni kweli. I—imani yako iligusa kitu fulani.

214 Vipi ninyi, pande *hizi* huku, mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Naam."—Mh.] Iweni na imani, basi. Msiwe na shaka.

215 Hapa, bibi huyu anayeketi hapa aliyevaa kofia nyeusi, amevaa miwani. Una kadi ya maombi, bibi? Papo hapo nyuma ya huyo mvulana mdogo pale, mwisho wa safu, wewe! Una kadi ya maombi? Huna kadi ya maombi. Unaamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Kama Mungu atanifunulia kwamba shida yako ni

nini, basi je! utakubali jambo hilo basi? Una shida ya moyo. Huyo ni mume wako anayeketi karibu na wewe, naye ana shida ya tezi. Sasa enendeni zenu na mwamini.

Ni nani anayemwamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

216 Vipi kuhusu mwanamume huyu mweusi anayeketi hapa? Je! unaamini, bwana? [Mtu huyo anasema, "Ndiyo, bwana."—Mh.] Unaamini kwamba mimi ni mtumishi Wake? ["Ndiyo."] Unataka maombi, sivyo? ["Ndiyo."] Kama Mungu atanifunulia, kutoka kwangu kuja kwako, unamwamini Yeye. . . ya kwamba ungeweza kulikubali? ["Ndiyo."] Una shida ya mbweta. ["Ndiyo, bwana."] Na una shida ya kutokeza utumbo. ["Ndiyo."] Hiyo ni kweli.

217 Vipi ye yote wenu hapo, je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

218 Kuna mwanamke mwingine mweusi nyuma tu ya bibi huyu hapa nyuma. Umeinua mkono wako, dada. Unataka jambo fulani kutoka kwa Bwana? Unaamini kwamba mimi ni mtumishi Wake? Ni ugonjwa wa sauti, unaougua. Hiyo ni kweli. Unaamini Yeye alikuponya?

219 Moja kwa moja kutoka kwako pale, unayeangalia upande huo, papo hapo kutoka hapo ulipo mwisho wa safu; kama mtu mmoja, wawili, watatu, wanne, watano kule nyuma. Una shida ya kikoromeo. Unaamini ya kwamba Mungu atakufanya mzima?

220 Vipi papa hapa nyuma? Mwanamume aliyeko kule mwisho wa kiti, papa hapa nyuma kwenye safu hii. Una uvimbe wa utumbo mpana. Hiyo ni kweli, bwana. Unaamini ya kwamba Mungu anakuponya? Basi simama na ukubali jambo hilo, katika Jina la Bwana Yesu.

221 Mungu akubariki. Sijapata kukuona. Wewe ni mgeni kwangu. Bali Mungu anakujua.

222 Unaamini jambo hilo, kila mmoja wenu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Je! unaamini Malaika yule yule wa Mungu aliyemjia Ibrahimu, katika rehema, Ambaye alijua siri za mawazo ya Sara, yeye yule aliyesimama duniani na kujua siri za moyoni, je! huamini Yeye yuko hapa sasa? ["Amina."] Mungu yeye yule, kabla tu ya ulimwengu kuteketezwa tena katika maangamizi, je! wewe huamini Yeye yuko hapa? ["Amina."] Basi hebu tumkubali. Hebu na tumwamini. Hebu na tumchukue kama mponyaji wetu, sasa hivi. Ni wangapi wenu wataamini jambo hilo?

223 Ni wangapi wenu wanaoamini kweli kweli? Inueni mikono yenu. Sasa, wekeni, wekeni mikono yenu chini.

224 Biblia ilisema hivi, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

225 Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi, basi, kama ninyi ni waamini. Mwombee mtu aliye karibu na wewe. Ndipo yule aliye karibu na wewe, akuombee wewe unayeombewa. Kila mmoja wenu, ombeaneni sasa, po pote humu jengoni. Ninaisai imani hii.

Yule bibi pale aliye na TB, isahau. Umeponywa.

226 Wewe uliye na shida ya kibofu, unayeketi pale, bwana, unayeamka usiku. Sahau hilo. Haitakulazimu kufanya hivyo tena. Mungu akubariki.

227 Ninawasai kufanya tendo la kuamini. Mtafanya hivyo? Basi ombeni, kila mmoja wenu, katika njia yenu wenyewe. Mwekee mikono mtu fulani na umwombee mtu aliye karibu nawe, wakati nikiwaombea ninyi nyote.

228 Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, mwazilishi wa Uzima wa milele, mpaji wa kila kipawa chema, mtume Roho Wako hivi sasa juu ya watu hawa.

229 Ninalaani kazi za Ibilisi, kwa maana Ibilisi amefichuliwa. Shetani, huwezi kuwashikilia tena. Imani yao inaongezeka, nao wamewekena mikono. Nami ninakusai, ya kwamba umepoteza vita, na hukumu imekaribia. Watoke, katika Jina la Yesu Kristo. Ondoka kwao, katika Jina la Yesu.

230 Mnamwamini? Inueni mikono yenu na mumpe sifa kwa ajili ya kuponywa kwako. Kama wewe ni kiwete, simama kwa miguu yako; Kristo anakuponya. Kama wewe umelemaa, mikono yako imelemaa, iinue juu; yote yamekwisha.

Huyu hapa mwanamke aliye kiwete, akisimama.

231 Bwana asifiwe! Hebu na tuseme, "Bwana asifiwe," kila mtu. [Kusanyiko linasema, "Bwana asifiwe!" Ndugu Branham anapiga makofi mara tano—Mh.] Amina.

Ndugu Neville.

JE! KANISA LITAONDOKA KABLA YA ILE DHIKI? SWA58-0309E
(Will The Church Go Before The Tribulation?)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, 09 Machi, 1958, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2003 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2003 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org